SHULA YA SEKONDARI MARATA
S. L. P 544
NANYUMBU
TAR:…………………………..

JINA LA MWANAFUNZI:………………………………………………………………………………………………..

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MARATA ILIYOPO WILAYA YA NANYUMBU MKOA WA MTWARA MWAKA……………….**

## 1.0. UTANGULIZI.

Ninafuarahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2021. Shule ya sekondari Marata ipo umbali wa Km 55 toka makao makuu ya Wilaya ya Nanyumbu ( Upande wa Kusini Magharibi) na Km 35 toka Mji wa Masasi. Shule ipo katika kijiji cha Maratani, Kata ya Maratani, tarafa ya Maratani.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 ndani ya siku saba baada ya hapo hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa kushindwa kumleta mwanao shuleni kwa wakati. Ni vizuri kuwahi kufika shuleni ili mwanafunzi aweze kuendana na mpango kazi wa shule.

## 2.0. MAMBO YA KUZINGATIA.

2.1. Sare za Shule.

a. Sare za Shule ni kama ifuatavyo:-

1. Kwa wavulana.
    - Suruali yenye linda rangi ya dark blue ziwe mbili (2).
    - Shati jeupe la mikono mifupi. Yawe mawili (2) (Tetron)
    - Tisheti rangi ya dark blue.
    - Viatu vyeusi vya ngozi pea mbili.
    - Soksi nyeupe pea mbili.
2. Kwa wasichana.
    - Sketi mshono wa rinda boksi rangi ya dark blue. Ziwe mbili (2)
    - Gauni ya kazi za nje rangi ya damu yam zee moja (1)
    - Shati jeupe mikono mifupi. Yawe mawili (2) au Nusu kanzu rangi nyeupe ziwe mbili (2) (Tetron)
    - Tisheti ya rangi ya dark blue.
    - Kwa watakaovaa Hijabu, rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sare za shule.
3. Sare za Michezo kwa wavulana.
    - Jezi ya blue na raba
    - Traki suti ya bluu na raba
    - Vitambaa vya sare vya shule vinapatikana shuleni
4. Sare ya michezo kwa wasichana
    - Traki suti ya bluu na raba

## 4.0. VIFAA VINGINE MUHIMU VYA MWANAFUNZI

1. Counter book $Q^2$ kumi (10)
2. Daftari kubwa za mazoezi kumi (10)
3. Kalamu na mkebe wa hesabu
4. Kamusi (Dictionary) Oxford
5. Rim paper moja (1)
6. Bima ya afya

## 4.0. VIFAA VYA USAFI

- Ndoo ndogo moja (1)
- Fagio la chelewa (makuti)
- Jembe moja (1)

**5.0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII**

Shule hii inaendeshwa na sheria pia inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
f) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
h) Kutunza mali za umma

**6.0. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

a) Wizi
b) Usharati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya uma
g) Kudharau bendera ya Taifa
h) Kuoa au kuolewa
i) Kutoa mimba
j) Kugoma, kuchochea na kuongozana au kushiriki kuvuga amani na usalama wa shule au watu
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kuwa na simu ya mkononi.

**7.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

a) Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule Marata utakaporipoti shuleni.
b) Vifaa vyote vilivyoagizwa mwanafunzi anapaswa aje navyo shuleni siku ya kuripoti ili vikaguliwe

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA

JINA LA MKUU WA SHULE: SIMON M. MPANGENI SAHIHI…………………………..

NAMBA YA SIMU: 0786 943 322/ 0621 558 735

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFIS YA RAIS-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU**
**SHULE YA SEKONDARI MARATA**

**<u>FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA MARATA</u>**

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

i. Mimi……………………………………………………………………………..ninakubali kuingiakidato cha …………………………..katikashuleyasekondariya ……………………………………………Tarehe…….……………………….. Nitafikashulenibilakuchelewananaahidikwambanitakuwamwanafunzi bora mwenyebidiinautiimudawotenitakaokuweposhuleni.

ii. Anuaniyanguyakudumuni………………………………………………………..… …………………………………………………………………………………………

iii. Sahihiyamwanafunzi……………………………………………………………

**B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi……………………………………………………………….nakubali/sikubalimtotowangu ……………………………………………………………ajiungenashuleyasekondariMaratani kuanziatarehe……………………………..naahidivituvyoteanavyotakiwakufikanavyoshulenivilivyo tajwakatikabaruahii.

Nitahakikishakwambamtotowanguamesomasheriazotezashulenakuzielewaameahidimbeleyangukuwaatakuwamtiifunamwenyebidiikazininadarasani.
Mtotowanguakiwashulenialelewekatikadiniya ……………………………………...

**SimuNa**…………………………………………………………………………………..

**Sahihiyamzazi/mlezi**……………………………………………………………………

**MUHIMU:**
***Tafadhalifomuhiiirudishweshulenikablamtotowakohajaondokanyumbani au ajenayosikuya kwanza anapokuja.***